



## PRESS STATEMENT: 10 AGOSTI 2016



### SEEDS OF FREEDOM DOCUMENTARY LAUNCHES TODAY

Dar es Salaam - 10 Agosti, 2016 -

Tanzania Organic Agriculture Movement (TOAM), shirika mwanvuli la kilimo hai Tanzania, leo, linazindua filamu ya Uhuru wa mbegu za wakulima nchini.

*Uhuru wa mbegu za wakulima* imerekodi shuhuda za wakulima ambao haki zao za kimila za kutunza, kushirikishana na kubadilishana mbegu, zinatishiwa na uwepo wa sheria zinazozipa kipaumbele mbegu za chotara kuchukua nafasi ya mbegu za asili na kuyakabidhi makampuni makubwa ya mbegu haki ya kumiliki na kuzalisha mbegu. Filamu hii ya dakika 28, inamfuatilia, ndugu Mathias Mtwale, mzalishaji wa ndani wa mbegu katika safari yake ya kukutana na wakulima, watafiti, wasambazaji wa mbegu na watunga sheria ili kuelewa suala hili na kuweka ushawishi wa haki kwa ajili ya wakulima.

*"Tumekutana na wadau tofauti katika mfumo wa mbegu, hasa wakulima, ili kujionea jinsi sera na sheria zinavyowaweka kwenye tabaka la chini, kwa kuyapa kipaumbele makampuni makubwa na wale wote wenye nguvu za kiuchumi kumiliki mfumo wa kuzalisha mbegu"*, anasema: Ndugu Mtwale.

Filamu hii inaweka wazi ukweli kuhusu mfumo wa mbegu Tanzania. Inatukutanisha na wakulima wa Morogoro, Dodoma na Lushoto ambao, wanatupa simulizi za kusimua kuhusu mbegu za asili na jinsi zilivyorithishwa kuitia vizazi tofauti. Watafiti nao, wanaelezea namna

mfumo wa mbegu za kibiashara za chotara usivyokidhi mahitaji ya wakulima. Mashirika ya wakulima yanaainisha namna mfumo mpya wa sheria wa kusimamia mbegu unavyokuwa na madhara kwa bioanuai tajiri ya kilimo iliyotunzwa na wakulima wadogo.

*“Mbegu hizi ni urithi wetu, na tutazirithisha kwa watoto wetu na wajukuu wetu. Pia, hizi ni mbegu bora na ni fahari ya watanzania. Lakini sheria zetu haizilindi mbegu hizi,”* anasisitiza Janet Maro, ambaye ni Mkurugenzi wa Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), ya Morogoro.

Profesa Joseph Hella, Mkufunzi kutoka chuo kikuu cha Sokoine, pia anahimiza, “Juhudi yoyote ya kuboresha kilimo hapa Tanzania hutegemea zaidi namna tunavyoboresha mbegu za asili wanazomiliki wakulima.”

Filamu hii, ambayo, imeandaliwa na mshindi wa nishani wa Sweden, Mkurugenzi Lars Johansson na Mtengenezaji filamu mzoefu Mtanzania, Bw. Suleyman Kissoky, inazinduliwa leo, Jumatano, tarehe 10 August, 2016. The film was produced with the support of the Rosa Luxemburg Stiftung with funds from German Federal Ministry for Economic Cooperation and Development (BMZ).

Unaweza kuangalia filmu hii hapa: <https://uhuruwambegu.wordpress.com>  
na kurasa za Facebook: Tanzania Organic Agriculture Movement –TOAM, Tanzania Alliance for Biodiversity

#### MWISHO

Kwa taarifa zaidi na/au mahojiano, tafadhali wasilianana na:

- Bw. Abdallah Mkindi, Mratibu wa TABIO, [tabiosecretariat@gmail.com](mailto:tabiosecretariat@gmail.com), +255 784 311 179 au
- Bw. Anatory Gabriel, wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa TOAM, [anatorygabriel@yahoo.com](mailto:anatorygabriel@yahoo.com), +255 768 909 055.

Tanzania Organic Agriculture Movement (TOAM) ni shirika mwavuli la sekta ya kilimo hai hapa nchini. [www.kilimohai.org](http://www.kilimohai.org)

Tanzania Alliance for Biodiversity (TABIO) ni mtandao wa mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi ambayo yanaguswa na utunzaji wa bioanuai ya kilimo kwa usalama wa maisha na uhuru wa chakula.